**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA TABORA**

*Unapojibu tafadhali taja:*
**Kumb.Na.**TMC/U/371/15 **Tarehe:** 24.06.2025

**YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.**

Halmashauri ya Manispaa ya Tabora inapenda kuwatangazia Watanzania wote nafasi za kazi za ajira ya mkataba wa muda wa mwaka mmoja (1) katika nafasi za Wakusanya Mapato, Migambo na Madereva daraja la II.

**1. WAKUSANYA MAPATO 35.**

**2.1 SIFA ZA MWOMBAJI**

Mwombaji anatakiwa awe na sifa zifuatazo:-

i. Awe na Elimu ya kidato cha Nne (IV) au cha sita (VI) na mwenye Ujuzi.
ii. Awe amehitimu Mafunzo ya Astashahada (Certificate) na Stashahada ya Uhasibu, TEHAMA, Utawala wa Biashara na Manunuzi ya Umma.
iii. Awe Mwadilifu na ambaye hajawahi kukutwa na Hatia Mahakamani,
iv. Awe na Mdhamini Mwenye makazi yake Halmashauri ya Manispaa ya Tabora na mwenye mali Isiyohamishika.

**2.2 KAZI/MAJUKUMU YA WAKUSANYA MAPATO**

i. Kukusanya mapato kwenye chanzo alichopangiwa kwa mujibu wa Sheria Taratibu na Kanuni.
ii. Kuandaa/kuhuisha kanzi data ya chanzo cha mapato atakachopangiwa.
iii. Kutoa taarifa ya ukusanyaji kila siku baada ya kukusanya mapato.
iv. Kutunza vitendea kazi (POS) atakayopatiwa na Mwajiri kwa mujibu wa maelekezo atakayopewa
v. Kuweka fedha Benki kila siku baada ya makusanyo.
vi. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi.

**3.0 DEREVA DARAJA LA II- NAFASI 7**

**3.1 SIFA ZA MWOMBAJI**

i. Awe na elimu ya kidato cha Nne (IV) au Sita (VI).

ii. Awe na elimu ya kidato cha Nne (IV) na Leseni ya Daraja E au C1 ya uendeshaji wa Magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja (1) bila kusababisha ajali.

iii. Awe amehudhuria mafunzo ya Msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha mafunzo ya ufundi stadi (VETA) au kingine kinachotambuliwa na Serikali.

v. Waombaji wenye cheti cha majaribio ya ufundi daraja la II watafikiriwa kwanza.

## 4.0 KAZI/MAJUKUMU YA DEREVA DARAJA LA II

i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
iii. Kufanya matengenezo madogomadogo ya gari.
iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.
vi. Kufanya Usafi wa Gari.
vii. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake wa kazi.

## MGAMBO-NAFASI 26

## 5.0 SIFA ZA MWOMBAJI.

Mwombaji anatakiwa awe na sifa zifuatazo:-

i. Awe na elimu ya kidato cha Nne (IV) au Sita (VI).
ii. Awe amehudhuria na kuhitimu mafunzo ya Mgambo.
iii. Awe Mwadilifu na ambaye hajawahi kukutwa na Hatia Mahakamani.

## 5.1 KAZI/MAJUKUMU YA MGAMBO

i. Kuhakikisha kwamba mali yeyote ya Ofisi inayotolewa langoni (nje ya ofisi) ina hati ya idhini.
ii. Kuhakikisha kuwa mali yote inayoingizwa langonioo inazo hati za uhalali wake.
iii. Kulinda usalama wa majengo, ofisi na mali za ofisi mchana na usiku.
iv. Kuhakikisha kwamba milango na madirisha yote yamefungwa ipasavyo mwisho saa za kazi.
v. Kuhakikisha kwamba wageni wote wanaoingia katika eneo la ofisi wana idhini ya kufany hivyo.
vi. Kupambana na majanga yoyote yatakayotokea katika sehemu ya kazi kama vile moto, mafuriko na kutoa taarifa katika vyombo vinavyohusika kama vile Polisi na Zimamoto.
vii. Kutoa ushauri wa jinsi ya kuboresha huduma ya ulinzi mahali pa kazi.
viii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi.

**6.0 MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI.**

i. Mwombaji awe na umri kati ya miaka 18 hadi 45 (Ambatanisha cheti cha Kuzaliwa) na lazima awe raia wa Tanzania.
ii. Mwombaji wa ajira analazimika kuwa na namba ya utambulisho wa uraia (National Identification Number) kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).
iii. Maombi yaambatanishwe na nakala za vyeti vya taaluma na mafunzo vilivyothibitishwa – **Result Slip hazikubaliki**, Cheti cha kuzaliwa, Maelezo binafsi (Curriculum Vitae) Picha Ndogo za Rangi (Colored Passport Size) mbili (2).
iv. Waombaji wenye sifa pungufu au zaidi ya zilizotajwa hapo juu hawashauriwi kuomba.
v. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU au NECTA)
vi. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama ana kibali cha Mamlaka husika.
vii. Mwombaji awe hajawahi kupatikana na hatia ya kosa la jinai na kufungwa jela.
viii. Katika barua ya maombi, weka namba za simu zinazopatikana muda wote.
ix. Waombaji watakaokidhi sifa na vigezo watajulishwa tarehe ya usaili.
x. Mshahara kwa kazi zote za mkataba ni kima cha chini cha Serikali (kabla ya mwezi Julai, 2025).
xi. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 09.07.2025 saa 9:30 alasiri
xii. Maombi yote yatumwe kwa Anuani ifuatayo.
xiii. Kwa waombaji walio na kazi hii ya mkataba wanaruhusiwa kuombe

Ofisi ya Mkurugenzi,
Halmashauri ya Manispaa ya Tabora,
4 Barabara ya Kiwanja cha Ndege,
S.L.P 174,
**45182 TABORA**

Tangazo hili linapatikana katika tovuti ya Halmashauri ya Manispaa ya Tabora www.taboramc.go.tz na barua pepe md@taboramc.go.tz na kwenye mbao za matangazo.

Dkt. Shani J. Mudamu
**KAIMU MKURUGENZI WA MANISPAA**
**TABORA**

MKURUGENZI WA MANISPAA
S. L. P. 174
TABORA